Swahili

# Maelezo kwa ajili Yako







## Brosha hii inahusu:

- haki na wajibu wako
- faragha yako na maelezo ya kibinafsi
- jinsi ya kutoa maoni au kuwasilisha malalamiko
- jinsi ya kupata mtu wa kukuwakilisha na kukusaidia

Una haki na wajibu wakati unapopokea huduma zetu.

Tunatarajia wafanyakazi, wafanyakazi wa kujitolea na wateja na watunzaji wao kuheshimiana.

## Maelezo yako yamelindwa vyema

Tumejitolea kuhakikisha kuwa maelezo yako yanatunzwa kwa faragha. Faragha yako inalindwa pia na sheria. Tunalinda maelezo yako chini ya kiwango cha juu cha usalama.

Ikiwa unahitaji, unaweza kuona maelezo yako ya afya. Una haki ya kuomba kuona rekodi yako ya huduma za afya na kuomba irekebishwe ikiwa si sahihi.

## Picha za afya au rekodi ya sauti

Baadhi ya wafanyakazi wa afya wanaweza kuhitaji kupiga picha kama sehemu ya utunzaji wako, au kurekodi sauti yako. Ikiwa UNAKUBALI hatua hii, utaandika jina lako kwenye fomu ya idhini katika rekodi yako ya huduma za afya.

.



# Je, tunakusanya maelezo gani ya kukuhusu?

Tunahifadhi jina lako na maelezo ya mawasiliano kwenye rekodi yako ya kibinafsi ya afya. Maelezo kuhusu afya yako ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu hali yako, mpango wako wa utunzaji na maendeleo ya matibabu yanaandikwa katika rekodi yako ya huduma za afya kila unapotembelea kituo.

Kukusanya maelezo hutusaidia kuweka maelezo sahihi kuhusu mahitaji yako, ili tuweze kukusaidia kwa njia bora zaidi iwezekanavyo.

Tunaripoti pia maelezo ya jumla kwenye Idara ya Afya. Hii husaidia katika kupanga na kuboresha huduma zetu.

Hatushirikishi maelezo yoyote ambayo yanaweza kutumika kukutambulisha.

Maelezo yako yanaweza kuonekana tu na wafanyakazi wa IPC Health wanaohusika katika utunzaji wako. Tunashiriki maelezo yako na wafanyakazi wengine tu ikiwa unakubali au ikiwa sheria inatuamrisha, kama vile katika dharura ya matibabu.



Una usemi katika kile kinachotokea kuhusiana na maelezo yako.

Hatutashirikishi maelezo yako na mtu yeyote isipokuwa kama:

- utatoa idhini (unakubali)
- utatuomba tushiriki maelezo hayo
- maisha yako, au maisha ya mtu mwingine, yako hatarini
- tunadhani kuwa kuna tishio kubwa kwa usalama au ustawi wa watoto au familia zao
- ni kwa manufaa yako
- sheria inatuamrisha kufanya hivyo, kwa mfano kwa magonjwa ya kuambukiza na aina fulani za saratani, au kesi fulani zinazosikilizwa na mahakama

Una haki ya kutoshiriki baadhi ya maelezo yako au kuweka kikomo cha wale wanaoona rekodi yako ya huduma ya afya. Hata hivyo, hatua hii inaweza kufanya iwe vigumu kwetu kukupa huduma bora zaidi.

Wasiliana nasi ikiwa ungependa kubadilisha au kughairi idhini yako.

Una haki ya kukubali au kukataa matibabu.

Mhudumu wako wa afya akishakueleza hali yako (zako) na matibabu yanayoweza kutumiwa kwa hali hii (hizi) unaweza kuchagua kutoa idhini au kukataa matibabu. Utaandika jina lako kwenye fomu ya idhini katika rekodi yako ya huduma ya afya karibu na chaguo lako; kwa mfano, kukataa au kukubali matibabu.

# Haki na wajibu wako

## Unachoweza kutarajia kutoka kwetu:

- utatendewa kwa upole na heshima
- utapokea huduma ya hali ya ubora wa juu
- desturi na imani zako za kikabila, kitamaduni na kidini zitaheshimiwa
- utapokea maelezo ambayo unaweza kuelewa na unaweza kupata mkalimani ikiwa unamhitaji
- utapewa maelezo yatakayokusaidia kufanya maamuzi kuhusu jinsi ya kuboresha afya yako
- utatathminiwa kwa haki kuhusiana na huduma unazohitaji
- utahusishwa katika maamuzi ya kuhusu utunzaji wako
- maelezo yako ya kibinafsi yatatunzwa kwa faragha
- unaweza kuomba nakala ya maelezo yako ya kibinafsi
- ruhusa (idhini) yako itachukuliwa kabla hatujashiriki maelezo yako ya kibinafsi na huduma zingine zozote
- unaweza kuomba mabadiliko ya mfanyakazi
- unaweza kukataa matibabu
- unaweza kukataa huduma ikiwa hungependa kupokea huduma hiyo sasa na unaweza kutufahamisha utakapokuwa tayari
- unaweza kukataa kuwepo kwa mwanafunzi au mtafiti chumbani wakati wa miadi yako
- unaweza kutupa maoni ya kweli na kuendelee kutumia huduma zetu
- tunaweza kuchagua mtu wa kukuwakilisha na kukusaidia (mtetezi) ikiwa unahitaji
- unaweza kumjumuisha mwenzi wako katika utunzaji wako

## Unachohitaji kujua:

- ukichelewa kufika kwenye miadi, huenda tusiweze kukupa huduma kamili kwa wakati huo
- huenda tusiweze kuendelea kukupa huduma ukikosa miadi bila kutufahamisha
- tunaweza kukataa kutoa huduma kwako ikiwa:
    - umelewa au ikiwa uko chini ya athari ya dawa za kulevya
    - una ujeuri na unawatusi wafanyakazi
    - utatishia kuumiza mtu yeyote
    - utamnyanyasa mtu yeyote kingono

## Tunachotarajia kutoka kwako:

- kufika kwenye miadi yako kwa wakati
- ikiwa huwezi kufika kwa miadi yako, tafadhali tujulishe angalau siku moja kabla ya miadi
- kuwa na heshima na adabu kwa kila mtu unayekutana naye unapopokea huduma zetu
- kuomba maelezo zaidi ikiwa huelewi, hasa ikiwa unahitaji kutoa idhini yako kwa matibabu fulani
- ikiwa wafanyakazi wetu wanatembelea nyumba yako, tafadhali hakikisha kuwa ni salama kwao kuweza kuja. Hii ni pamoja na kuwaweka wanyama wa kufuga kipenzi mbali na kutovuta sigara wakati wafanyakazi wetu wako pamoja nawe
- kufuata ushauri ambao mhudumu wako wa afya anakupa kadri ya uwezo wako
- hatuwezi kukusaidia ikiwa hutatuambia vitu ambavyo maelezo tunayohitaji kujua kuhusu afya yako
- kutusaidia kuhakikisha kuwa majengo yetu ni mahali salama kwa kila mtu:
- kuheshimu watu wengine na faragha yao wakati wote
- kutufahamisha maelezo yako ya kibinafsi yanapobadilika
- kutunza vitu unavyoazima kutoka kwetu kwa malengo ya matibabu



# Utetezi

Mtetezi ni mtu anayekusaidia ili kuhakikisha kuwa unapata huduma unazohitaji. Wanaweza kukusaidia pia kuelewa haki na wajibu wako kuhusu afya yako.

Mtetezi anaweza kuwa:

- rafiki
- mwanafamilia
- mtu anayetoka katika huduma ya utetezi

IPC Health itakuwa radhi kwako kuomba mtetezi. Tutakusaidia kupata mtetezi anayekufaa.

Ikiwa ungependa rafiki au mwanafamilia ahudhurie miadi yako au ahusishwe katika utunzaji wako, tafadhali zungumza na mfanyakazi wako wa IPC Health.

Unaweza kuwasiliana pia na huduma ya utetezi na uwaombe wakupe mtetezi.

# Huduma za utetezi

**Simu ya Ofisi ya Mtetezi wa** Umma: 1300 309 377
publicadvocate.vic.gov.au

**Utetezi wa utunzaji wa wazee Nambari ya simu isiyolipishwa:**
1800 200 422
myagedcare.gov.au

**Utetezi wa Haki za Wazee Nambari ya simu isiyolipishwa:**
1800 700 600
era.asn.au

**Utetezi wa Watu Walio na Ulemavu wanaotoka katika Jumuiya za Kikabila Nambari ya simu isiyolipishwa**
1800 626 078
adec.org.au

## Nambari zingine muhimu

**Simu ya Kamishna wa Malalamiko ya Afya:**
1300 582 113
hcc.vic.gov.au

**Simu ya Ofisi ya Kamishna wa Maelezo wa Australia**
1300 363 922
oaic.gov.au

**Simu ya Idara ya Familia, Haki na Makazi:**
1300 475 170
dffh.vic.gov.au

**Simu Idara ya Afya**
1300 650 172
health.vic.gov.au

**Nambari ya simu isiyolipishwa ya Ombudsman wa Victoria**
1800 806 314
ombudsman.vic.gov.au

**Simu ya Tume ya Victoria ya Fursa Sawa kwa Wote na Haki za Binadamu:**
1300 292 153
humanrightscommission.vic.gov.au

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na kituo cha IPC Health kilicho karibu nawe kilichoorodheshwa nyuma ya brosha hii.

## Maoni


Tungependa kupata maoni yako kuhusu huduma na vituo vyetu. Tunategemea maoni yako ili kuboresha huduma zetu.

- unaweza kuandika maoni na kuyaweka kwenye kisanduku cha maoni kwenye chumba cha kusubiri
- unaweza kuzungumza na mfanyakazi yeyote ana kwa ana au kwa njia ya simu
- tunaweza kukuomba ujaze Utafiti wa Maoni ya Mteja kuhusu huduma zetu. Utafiti huu unauliza maswali ili kutusaidia kupanga na kukagua huduma zetu
- unaruhusiwa kuja na mtu yeyote ili kukusaidia ikiwa ungependa kujadili maswala yoyote kuhusu huduma
- ikiwa hupendezwi na sehemu yoyote ya huduma, unaweza kuwasilisha malalamiko rasmi. Piga simu kwa kituo cha IPC Health ulichohudhuria na uombe kuzungumza na meneja wa mpango, mkurugenzi au afisa mkuu mtendaji
- unaweza kuwasiliana pia na Kamishna wa Malalamiko ya Afya kwa **1300 582 113**

## Je, una maswali mengine yoyote?

Tafadhali zungumza na mmoja wa wafanyakazi wetu wa IPC Health ikiwa una maswali mengine yoyote kuhusu kile kinachotokea kwa maelezo yako wakati unapokea utunzaji wetu, au ikiwa ungependa kuona rekodi yako ya huduma za afya.

Ili kupata nakala ya Sera ya Faragha ya Maelezo, tembelea **humanservices.gov.au/customer/privacy**



**Ofisi Kuu ya IPC Health**

106 Station Road
Deer Park VIC 3023
PO Box 171 Deer Park VIC 3023

**ACN** 136 685 151
**ABN** 68 846 923 225

**Deer Park**

106 Station Road
Deer Park 3023

**St Albans**

1 Andrea Street
St Albans 3021

**Sunshine**

Level 1, 499 Ballarat Road
Sunshine 3020

**Altona Meadows**

330 Queen Street
Altona Meadows 3028

**Hoppers Crossing**

117–129 Warringa Crescent
Hoppers Crossing 3029

**Wyndham Vale**

510 Ballan Road
Wyndham Vale 3024

**1300 472 432**

**W** ipchealth.com.au
**E** ipchealth@ipchealth.com.au

IPC Health   IPC Health   IPCHealth_au